# Meya Dar kukutana na mmiliki wa UDA

■ Edith Msuya

MEYA wa Jiji la Dar es Salaam, Isaya Mwita amepanga kukutana na mmiliki wa Hisa za Shirika la Usafirishaji la Jiji la Dar es Salaam (UDA), Simon Group Limited (SGL), Robert Kisena ili kuzungumza naye kibiashara na uhalali wa hisa hizo.

Akizungumza na gazeti hili, Mwita alisema lengo la kukutana na mfanyabiashara huyo ni kujadiliana mambo mbalimbali kuhusu hisa hizo ambazo aliuziwa.

"Tunataka tukae naye ili kuzungumza naye kibiashara na kupata ufafanuzi juu ya uhalali wa hisa hizo alizouziwa kwani, suala hilo la Uda ni mali ya umma," alisema.

Mwita alisema wao wanashindwa kulifuatilia suala hilo kwani, tayari



Isaya Mwita

wamekosa nguvu kisheria, wakati hisa hizo zikiuzwa wao hawakuwepo.

Alisema pamoja na hayo pia, wanataka kumwomba mfanyabiashara huyo kuwasaidiaje katika suala hilo.

"Unajua hizi hisa zilizouzwa ni sawa na baba amefariki sasa amewaachia watoto shamba, wale watoto baada kukaa kwa pamoja wakagundua shamba lile limeuzwa, lakini si kihalali na aliyenunua anasema ameuziwa kihalali," alisema.

Awali, Baraza la Madiwani la jiji hilo lilibatilisha uuzwaji wa hisa za halmashauri ya jiji, asilimia 51 ya hisa zilizopo na kuzirejesha kwenye mamlaka ya jiji hilo kutoka kwa mmiliki wa sasa wa hisa hizo.

Baraza hilo lilibaini mnunuzi wa hisa hizo ambaye ni kampuni ya SGL, hakufuata taratibu katika mchakato wa kuzinunua na kubainika kuwepo kwa udanganyifu mkubwa katika umiliki wake.

Hata hivyo, Msajili wa Hazina aliwahi kusisitiza kuwa, Kampuni ya Simon Group ndiyo wenye hisa halali katika shirika hilo.



Rais mstaafu Jakaya Kikwete (katikati waliokaa), akiwa katika picha ya pamoja na baadhi ya washiriki wa mkutano wa tatu wa Sera za Mabadiliko ya Tabia Nchi ulioandaliwa na Taasisi ya Uongozi kwa kushirikiana na Climate Strategies baada ya kuufungua Dar es Salaam juzi. Kutoka kulia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mazingira na Muungano), January Makamba, Mwenyekiti wa mkutano huo, Chuks Okereke na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Taasisi ya Uongozi Profesa Joseph Semboja. (PICHA NA DOTTO MWAIBALE)

## Kanali mstaafu Kondo aonya kuhusu ubinafsi serikalini

■ Peter Akaro, TSJ

KANALI Mstaafu Dk. Haruni Kondo amesema ubinafsi na chuki iliyopitiliza kwa viongozi serikalini ni tishio na ugonjwa hatari kwa umoja, mshikamano na ustawi wa nchi yetu.

Akizungumza Dar es Salaam jana, Dk. Kondo alisema suala la ubinafsi lisipoangaliwa kwa makini na kupuuzwa, madhara yake yanaweza kuwa makubwa, hasa kipindi hiki serikali ya awamu ya tano ikidhamiria kuikomboa nchi kiuchumi.

Dk. Kondo alikuwa akifanya rejea kutoka kwenye kitabu kidogo kiitwachacho 'Tujisahihishe' kilichoandikwa na Baba wa Taifa Hayati Mwalimu Julius Nyerere mwaka 1962, ambacho kiliwaonya viongozi na wananchi juu ya madhara ya ubinafsi kwa nchi changa kama Tanzania. Dk. Kondo alisema wanasiasa hao ni uchwara na kazi yao kubwa ni kupandikiza mbegu ya fitina, chuki na husuda miongoni mwa wananchi ili kuleta vurugu.

"Watu hao ni mabingwa wa kukejeli, kudharau, kubeza, na kudhalilisha kila kitu kwa kudai hakuna jema lililofanyika," alisema.

Dk. Kondo alisema Rais John Magufuli alionesha kuchukizwa na tabia hiyo na kuanza kuchukua hatua ya kuirekebisha, lakini wanatokea wanasiasa uchwara wanaoponda na kubeza jitihada kubwa zinazofanywa na uongozi wa awamu ya tano.

## Daraja la Kigamboni laongeza msongamano wa magari

■ Hussein Ndubikile

KAMANDA wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Mohamed Mpinga amesema kukamilika kwa daraja la Kigamboni kumeongeza msongamano wa magari katika barabara ya Kilwa muda wa asubuhi na jioni.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kamanda Mpinga alisema msongamano wa magari umeongezeka katika barabara hiyo kutokana magari yaliyokuwa yakitumia Kivuko cha Feri kulitumia daraja hilo kama njia mbadala. "Awali, magari mengi yalikuwa yakipita Kigamboni hivi sasa yanapita darajani, asubuhi foleni huanzia Uhasibu tofauti na siku za nyuma iliyokuwa," alisema...

# Profesa Shivji kukabidhi vitabu Sekondari Tambaza